JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI
ZA MITAA MANISPAA YA KINONDONI

**SHULE YA SEKONDARI MBWENITETA**

Usajili NO.S.4133 ya Januari 2009.Motto ‘‘strive academically for better future’’
S.L.P.67337. Dar es Salaam. Mob: 0693338484/0714797986.

Kumb Na MTSS/ADM/ ___________
Jina la mwanafunzi ______________________________
Anuani S.L.P ___________________

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………..........................................................................**

**S.L.P ……………, Wilaya...................................., Mkoa...............................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MBWENITETA ILIYOPO MANISPAA YA KINONDONI LA DAR ES SALAAM MKOA WA DAR ES SALAAM KWA MWAKA WA MASOMO …………………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka …………… na atasoma tahasusi ya HGK/ HGL/HKL/ HGfa/ PCB/ CBG.

Shule ya Sekondari Mbweniteta ipo katika mkoa wa Dar es salaam, Wilaya ya Kinondoni, kata ya Mbweni, Mtaa wa Teta. umbali wa Kilometa KM (3) kutoka barabara ya Bagamoyo kwa usafiri wa daladala. Ukitokea kituo cha mabasi (daladala) cha Makumbusho au Tegeta panda mabasi yanayokwenda Mbweni. Kwa wanaotoka mikoani, panda daladala za kwenda Tegeta nyuki, halafu panda daladala za Kwenda Mbweni hadi shuleni Mbwenitetasekondari. Muhula wa masomo unaanza tarehe …………mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule **Tarehe ……………** mwisho wa kuripoti shule ni **Tarehe ……….**

***** Siku ya kuja shuleni uwe umevaa Track suit kama ilivyoagizwa hapa chini.**

**2. 0 MA MBO MUHI MU YA KUZIN G ATI A :**

## 1. SARE YA SHULE

i. Suruali mbili rangi ya **dark blue** (yenye marinda mawili na mkunjo chini) isiwe ya kubana kwa chini.
ii. Shati nyeupe mbili za mikono mirefu.
iii. Tai mbili (zinapatikana shuleni)
iv. T-shirt moja ya rangi ya kijivu (form six) ambayo inapatikana karibu na shule kwa itakayovaliwa siku ya jumanne na ijumaa.
v. Viatu vyeusi jozi mbili (vyenye kisigino) na vyakufunga na Kamba.

**SARE BAADA YA MUDA WA MASOMO.**

i. T-shet mbili nyekundu (form six ) isiyo na maandishi (zinapatikana shuleni).
ii. Track sut dark blue pair moja kwa ajili ya ya kujisomea usiku.
iii. Socks nyeusi pair tatu.
iv. Taa ya Torch kwaajili ya dharura (matumizi binafsi)
v. Suruali mbili nyeusi za kushindia baada ya masomo za kitambaa
vi. Nguo za michezo bukta na fulana (Taifa stars) yenye miraba ya blue na njano.

**MAHITAJI MENGINE MUHIMU**

**A: Vifaa kwa matumizi binafsi**

i. Mwanafunzi anatakiwa kuja na Bima ya afya
ii. Madaftari (counter book 4 quires , idadi ni kuanzia 7). Na madaftari madogo saba (7) ya kufanyia mazoezi .
iii. Begi la mgongoni la kubebea madaftari.
iv. Godoro la size 3 kwa sita (lenye cover) wa mbali wanaweza kuja kununulia Dar es Salaam.
v. Mashuka ya mawili (rangi ya light blue)
vi. Foronya moja.
vii. Chandarua moja cha duara rangi ya blue.
viii. Sahani, kikombe, kijiko, bakuli kwaajili ya chakula
ix. Ndoo mbili (lita 20 na lita 10) zenye mfuniko.
x. Kifaa cha kuhifadhia maji ya kunywa
xi. Trunker linalofungwa na kufuri kwaajili ya kuhifadhia vifaa.
xii. Mop 1, jembe 1, reki 1, mfagio mmoja wa ndani, na wa nje mmoja
xiii. Vitabu vya kujisomea kulingana na tahususi aliyochaguliwa mwanafunzi GS NA BAM ni lazima.
xiv. Raba kwaajili ya michezo
xv. Taulo na kandambili za kuogea
xvi. Scientific calculator kwa watakao somo la Geografia,Fizikia, kemia na Biolojia
xvii. Graph pad.
xviii. Dissecting kiti kwa wanafunzi wanaosoma Baiolojia.

**B: vifaa kwa matumizi ya shule**

i. Ream 2 (plane paper, size A - 4) kwa mwaka
ii. Spring file 3.

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha hizi ziingizwe bank kuanzia 01/07/2024 na siyo mwezi sita 2024 katika akaunti ya shule** (**Jina la akaunti ni MBWENITETA SECONDARY SCHOOL No** 20501100033 NMB **Mwanafunzi aje na Original pay slip aliyolipia kwa jinalakemwanafunzi.**

***** Aje na Picha 3 passport size alizopiga kwa shati jeupe na background ya Blue.**

**Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU**

- ✞ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ✞ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ✞ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi au kuvuka mpaka wa shule na Bweni.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni size ya brashi na zisiwe za mitindo.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xviii. Kumiliki simu.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai na mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iii. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**NB:**

1. **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOAINISHWA MWANZONI MWA FOMU JUU.**

2. **Kila Mwanafunzi aje na BIMA yake ya Afya. Au aje na Shs 54,500/= ili asaidiwe na shule kukatiwa Bima ya Afya.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

…………………

**YAHYA A. KIRONDO**
**MKUU WA SHULE**
**0693338484**

***Mbweniteta sec & High School***
***P.O BOX 67337***
***Dar es salaam***

**Kwa mawasiliano rasmi/ofisi ni**

1. **Mkuu wa shule** **0693338484/0714797986**
2. **Makamu mkuu wa shule** **0765303363/0711718432**
3. **Paton** **0626461632**

PICHA YA MWANAFUNZI

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MBWENITETA SHULE YA SEKONDARI,**

**S.L.P. 67337,**
**DAR ES SALAAM.**

Kumb Na MTSS/ADM/ **TAREHE:….. / ….. / 20……**

**JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………………………………**

**A. FOMU YA MWANAFUNZI KUKUBALI SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE**

**Mimi ……………………………………………………………………………….nakubaliana na sheria na taratibu zilizoorodheshwa Katika kipengere namba 3 kinachohusu sharia na kanuni za shule na kuzifuata katika kipindi chote nitakapokuwa nasoma shuleni Mbweniteta. Natambua pia kuwa** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. **25** ya mwaka **1978** na inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Natakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio kamilifu katika kila shughuli ndani na nje ya shule na Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (**Preparation**).
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule.
(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa. Viatu, sweta au jaketi lisilo sare ya shule vitachukuliwa na havitarudishwa.
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. Kila mwanafunzi awe na begi la mgongoni"**School Bag**" rangi nyeusi.
(i) Shule haitoi chakula maalum (**Special diet**).

**Sahihi ya Mwanafunzi………………………Tarehe….. / …. / 20…….**

**********************************************************************

**B. HATI YA MZA ZI KUKUBA LI MA SHA RT I YA SHULE**

**Mimi……………………………………..………………………… wa S. L. P. ………… wilaya ya ……………………..Mkoa……………….**

**Ni Mzazi/Mlezi wa………………………….…………………………nimeyasoma masharti yote ya mwanangu ya kujiunga na shule ya sekondari Mbweniteta. NINAKUBALIANA/SIKUBALIANI NAYO. Pia nitasimamia utekelezaji wa sheria za shule alizopewa. Najua pia simu, utoro na uchelewaji shuleni HAVIKUBALIKI**

**Sahihi…………………………… Sahihi ya dole gumba**

PICHA YA MZAZI/MLEZI

**Namba ya Simu ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………….........**

**Maelezo haya yamethibitishwa na :- Mi hur i hus i ka i gong we**

1. **Mtendaji wa Kata /Kijiji……………………Jina:…………………………………….Sahihi………………………Simu:…………………..**

2. **Mtendaji wa Kitongoji/ Mtaa………………… Jina:……………………………………Sahihi……………………Simu:…………………..**

**KINONDONI MUNICIPLE COUNCIL**
**SECONDARY EDUCATION DEPARTMENT**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MANISPAA YA KINONDONI

**SHULE YA SEKONDARI MBWENITETA**
Usajili NO.S.4133 ya Januari 2009.Motto ‘‘strive academically for better future’’
S.L.P.67337. Dar es Salaam. Mob:. 0693338484/07114797986.

STUDENT’S MEDICAL EXAMINATION
..............................................................................................................................................................................

Date ............................

**TO: THE MEDICAL OFFICER**

**HOSPITAL**.........................................................................................................................

Student’s Name......................................................................Age.................. Sex
Please examine the above named as to his/her fitness for appointment/re-engagement as a student at a student at MBWENITETA SECONDARY SCHOOL

**MED ICAL CER TIFI CA TION.**
**(To be completed by Medical Officer)**

(A) **PHYSICAL EXAMINATION**
- Height .........................................................................................
- Weight.........................................................................................
- Eye sight......................................................................................
- Hearing .......................................................................................

(B) **PAST HISTORY**
- Heart diseases ..............................................................................
- Drug allergy ................................... ..........................................
- Asthma ........................................... .........................................
- Pneumonia ......................................................................................

(C) **LABORATORY TEST**

| | |
|---|---|
| Stool | |
| Urine | |
| Widal test | |
| VRDL | |
| Blood: B/S | |
| Blood Group | |
| Hb | |
| Tuberculosis | |
| HIV | |

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for appointment/re-engagement are as above.
Name of Authorized Doctor.....................................................................................
Signature......................................... Designation....................................................
Date ........................................... Stamp.